TAPANET

# MPANGO MKAKATI

# 2025 - 2029

## Table of Contents

**DIBAJI** ........ i

**MUHTASARI** ........ i

**1. Sisi ni Akina Nani (Who We Are)** ........ 1

**2. Historia na Mustakabari wa TAPANET** ........ 6

**3. Malengo na Vipaumbele Vyetu** ........ 15

**4. Rasilimali na Uendelevu** ........ 26

**5. Mfumo wa Utekelezaji** ........ 29

**6. Matokeo (Athari)** ........ 34

### List of Figures

Mchoro 1: Muundo wa Utendaji ........ 4
Mchoro 2: Uchambuzi maswala ya nje (PESTEL) ........ 10
Mchoro 3: Uchambuzi wa Mambo ya ndani ........ 11
Mchoro 4:Dira, Dhamira na lengo ........ 16
Mchoro 5: Nadharia ya mabadiriko (ToC) ........ 17
Mchoro 6: Vipaumbele vya Mpango Mkakati ........ 18

**List of Tables**

Jedwari 1; Usimamizi wa Viashiria Hatarishi (Risks) ........ 24
Jedwari 2: Mpango wa Utekelezaji ........ 30
Jedwari 3: Mfumo wa Ufuatiliaji na tathimini ........ 35

# DIBAJI

*Kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi*

Kwa fahari kubwa na dhamira thabiti, ninawasilisha Mpango Mkakati wa Mtandao wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria Tanzania (TAPANET) wa mwaka 2025–2029 — ramani ya njia inayodhihirisha kwa mara nyingine tena dhamira yetu ya pamoja ya kuwawezesha wananchi kisheria, kukuza haki katika ngazi ya jamii, na kuhakikisha ustahimilivu wa taasisi.

Mpango huu umeibuka wakati ambapo mahitaji ya huduma za msaada wa kisheria zinazotolewa kwa kushirikisha jamii yanaendelea kuongezeka, hasa miongoni mwa makundi yaliyotengwa na yasiyohudumiwa ipasavyo katika maeneo mbalimbali ya Tanzania.

Katika kipindi cha miaka iliyopita, TAPANET imekua kutoka kuwa mtandao wa uratibu hadi kuwa sauti na jukwaa kuu la mashirika ya wasaaidizi wa kisheria. Mpango Mkakati huu unajengwa juu ya mafanikio hayo, ukizingatia uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mkakati uliopita na sasa unaweka ajenda ya kishujaa inayozingatia utoaji huduma kuzingatia taaluma, kufanya uchechemuzi wa sera, na kuhakikisha uimara katika janja ya kifedha.

Kama Mwenyekiti wa Bodi, ninavutiwa na moyo wa kujitolea wa wanachama wetu, ushirikiano tulioujenga, na jamii tunazozihudumia. Mpango huu unaakisi siyo tu sauti na vipaumbele vyao, bali pia unaelekeza njia za ubunifu, mabadiliko ya kidijitali, na ushirikishwaji jumuishi. Bodi itaendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wake, kuhakikisha kuwa mtandao wetu unawajibika katika majukumu yake, kubadilika kulingana na mazingira, na kuwa na matokeo yenye athari chanya kwa jamii.

Tuwe pamoja — imara, tukiwa na umoja, na mikakati madhubuti zaidi kuliko wakati wowote — katika kuifanya Tanzania kama sehemu ambayo, kila mmoja anapata haki yake.

**Nemence Irya**

**Mwenyekiti,**
**Bodi ya Wakurugenzi**
Mtandao wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria Tanzania (TAPANET)

# MUHTASARI

Mtandao wa Wasaidizi wa Kisheria Tanzania (TAPANET), ambao ni mtandao wa hiari unaojumuisha zaidi ya mashirika wanachama 170, unaanza awamu mpya ya kimkakati kwa kuzindua Mpango Mkakati wa 2025–2029. Ukijengwa juu ya tuliyojifunza kutoka kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, mpango huu unawakilisha mabadiliko ya kimfumo kuelekea utoaji wa msaada wa kisheria wa kitaaluma, endelevu, na wenye athari kubwa nchini Tanzania.


Mkakati huu umejengwa juu ya nguzo tatu kuu zinazohusiana na Utaalamu zaidi, Uchechemui, na Uendelevu. Vipaumbele hivi vinakusudia kuimarisha utoaji wa huduma za wasaidizi wa kisheria, kuingiza msaada wa kisheria katika mifumo ya kitaifa, na kuhakikisha ustahimilivu wa kifedha na kiutendaji kwa TAPANET na wanachama wake.

Kiini cha mpango huu ni dhamira ya kuwawezesha jamii zilizo pembezoni kudai haki zao na kupata haki. Kwa kuwekeza katika Mfumo wa Kitaifa wa kuwapatia vyeti Wasaidizi wa Kisheria, kupanua majukwaa ya kidijitali ya msaada wa kisheria, na kuboresha uwezo na uratibu wa wanachama, TAPANET inalenga kuinua ubora na uaminifu wa kazi za wasaidizi wa kisheria kote nchini.

Mkakati huu pia unaleta ubunifu mkubwa — ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Mfuko (fedha) wa Ubunifu wa Msaada wa Kisheria, mitindo mpya wa ushirikiano na wadau, na mfumo wa utendaji kazi unaolenga wanachama. Jitihada hizi zinakusudia kuhakikisha kuwa msaada wa kisheria haupatikani tu bali pia ni jumuishi, unaozingatia usawa wa kijinsia, na unaotegemea hali halisi za jamii za Kitanzania.

Ili kuhakikisha uwajibikaji na matokeo yanayopimika, mpango huu unajumuisha mfumo mpana wa Ufuatiliaji, Tathmini, na Kujifunza, unaolingana na malengo ya kitaifa ya msaada wa kisheria na viwango bora vya kimataifa. Kupitia uchechemuzi unaotegemea takwimu, ushirikiano wa kimkakati, na programu zinazobadilika kutokana na mahitaji, TAPANET itaendelea kuwa chachu ya uwezeshaji wa kisheria na mageuzi ya kisera.

Mpango Mkakati wa 2025–2029 ni zaidi ya njia — ni mwito wa kuchukua hatua. Unawaalika serikali, asasi za kiraia, washirika wa maendeleo, na jamii kushirikiana kujenga Tanzania yenye haki na usawa, ambapo tunataka kuona haki siyo kitu cha hisani bali ni haki ya kila mtu.



# 1. Sisi ni Akina Nani (Who We Are)

**1.0. UTANGULIZI**

Mtandao wa Wasaidizi wa Kisheria Tanzania (TAPANET) ni mtandao wa hiari wa mashirika ya kiraia (CSOs) yanayotoa msaada wa kisheria na elimu ya kisheria kwa jamii zilizo pembezoni nchini Tanzania. Tangu usajili wake mwaka 2010 chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, TAPANET umekua hadi kufikia wanachama 170 wanaotoa huduma za kisheria kote nchini. Mtandao huu umekuwa na mchango mkubwa katika kutetea huduma za wasaidizi wa kisheria na kushirikiana na wadau mbalimbali ili kufanikisha malengo yake, hivyo kuimarisha huduma za msaada wa kisheria nchini kote..

Mpango Mkakati wa TAPANET 2025–2029 unaleta njia iliyo na muundo thabiti zaidi, inayozingatia ushirikishwaji wa jamii na inayolenga uendelevu wa huduma za msaada wa kisheria nchini Tanzania. Tofauti na mipango iliyopita, mpango huu una vipaumbele vitatu vya kimkakati, ukisisitiza uendelevu na taaluma kama msingi wa utoaji wa huduma. Mabadiliko haya yanaonesha umuhimu wa ushiriki wa ngazi ya jamii, kuhakikisha kuwa jamii zilizo pembezoni zinahusishwa kikamilifu katika shughuli za utoaji wa msaada wa kisheria.

*Mpango Mkakati huu unaleta mambo matano ya mabadiliko makubwa: 1) Mfumo wa kitaifa wa uthibitisho wa wasaidizi wa kisheria, 2) Mfuko wa ubunifu wa msaada wa kisheria, 3) Zana ya ushirikishwaji wa wanachama wa TAPANET, 4) Jukwaa la kidijitali la msaada wa kisheria, na 5) Jukwaa la pamoja la uchechemuzi na Asasi za Kiraia (AZAKI).*


Ubunifu muhimu katika mpango huu ni msisitizo wa TAPANET juu ya utawala bora na uimara wa taasisi, kwa kuboresha uwajibikaji, uwazi, na ufanisi wa uongozi. Aidha, mpango huu umejumuisha mfumo kamili wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E), unaosisitiza matumizi ya ufuatiliaji wa wakati halisi na mbinu za kujifunza kwa kubadilika ili kuboresha tathmini ya athari na kufanya maamuzi sahihi.

Uendelevu wa kifedha ni nguzo kuu ya mpango huu, ukilenga kuipeleka TAPANET kutoka utegemezi wa wafadhili kuelekea mikakati ya uhamasishaji wa rasilimali mbalimbali, ikiwa ni pamoja na uchangishaji wa ndani, ushirikiano na shughuli za kuzalisha kipato. Mpango huu pia unakumbatia mabadiliko ya kidijitali kwa kuimarisha shughuli za uchechemuzi, ujenzi wa uwezo, na majukwaa ya kupata maarifa ili kuendana na mitazamo ya kisasa ya utoaji huduma za msaada wa kisheria duniani.

Kwa kuimarisha uchechemuzi wa sera, ushirikishwaji wa wanachama, na ubora wa huduma, mpango huu wa kimkakati unahakikisha TAPANET inaendelea kuwa nguvu inayoendeshwa na jamii katika kusukuma mbele ajenda ya upatikanaji wa haki.


### 1.1. Dira, Dhamira, na Tunu

***Dira:***



Mtandao imara wa kitaaluma wa wasaidizi wa kisheria unaoongoza upatikanaji wa haki endelevu kwa wote.

***Dhamira:***



Kama mtandao, TAPANET itaunganisha, kuratibu, na kuimarisha mashirika ya wasaidizi wa kisheria Tanzania Bara kwa kukuza taaluma, kuboresha uchechemuzi, na kujenga uwezo ili kuhakikisha upatikanaji wa haki sawa na endelevu kwa jamii zote.

*Tunu za Msingi:*



## 1.2. Madhumuni ya Mpango Mkakati

Mpango mkakati wa TAPANET unahudumia madhumuni mbalimbali. Unatumika kama ramani ya kuongozea katika kubuni na kutekeleza programu na shughuli za TAPANET, kuhakikisha zinaendana na dira na dhamira ya shirika. Mpango huu husaidia kubaini na kuweka vipaumbele katika matumizi ya rasilimali ili kuongeza athari za huduma za msaada wa kisheria na kusaidia maeneo yenye uhitaji mkubwa zaidi. Pia unalenga kukuza ushirikiano na ushiriki wa wanachama, wadau, na washirika, na hivyo kuimarisha juhudi za pamoja za kufikia malengo ya pamoja. Zaidi ya hayo, mpango huu unalenga kuimarisha ushiriki wa wanachama wa TAPANET katika shughuli na maamuzi ya mtandao huu.

Aidha, mpango huu unasisitiza umuhimu wa uchechemuzi wa sera kwa ajili ya kuathiri mifumo ya kisheria na kukuza haki kwa jamii zisizohudumiwa ipasavyo. Mpango mkakati pia unakuza uwajibikaji na uwazi kwa kuweka malengo wazi na viashiria vya utendaji ndani ya TAPANET na kwa wadau wake. Unahakikisha kuwa shughuli na juhudi zote zinafuata sheria na kanuni za msaada wa kisheria za kitaifa, kikanda na kimataifa, kwa viwango vya juu vya taaluma ya sheria.

Mpango huu unaeleza mikakati ya kuhakikisha uendelevu na ukuaji wa TAPANET, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa uwezo, uhamasishaji wa rasilimali, na maendeleo ya shirika. Hatimaye, mpango huu unatoa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini endelevu wa shughuli za TAPANET, unaowezesha kufanya marekebisho na maboresho kulingana na mrejesho na matokeo.

## 1.3. Upeo na Muda wa Utekelezaji (2025–2029)


Mpango mkakati wa mwaka 2025 hadi 2029 unaainisha kwa uwazi malengo ya TAPANET, mikakati, hatua kuu, mgao wa rasilimali, pamoja na ushirikishwaji wa wanachama na wadau. Kwa kulenga kuboresha wanachama wake, TAPANET inalenga kuelekeza juhudi zake katika maeneo yanayooana na dira na dhamira ya mtandao. Njia hii jumuishi inahakikisha kuwa malengo ya TAPANET yanapimika na yanaweza kufikiwa ndani ya kipindi kilichopangwa.

Mpango huu wa miaka mitano, kuanzia 2025 hadi 2029, umegawanywa katika awamu mbalimbali, kila moja ikiwa na matokeo mahususi na hatua za utekelezaji. Mapitio ya maendeleo yatafanyika mara kwa mara ili kupima mafanikio na kufanya marekebisho yanayohitajika. Mpango huu umeandaliwa kama ramani ya njia inayoiwezesha TAPANET kufikia malengo yake makuu huku ikibakia na uwezo wa kuendana na mabadiliko yatakayojitokeza katika kipindi cha utekelezaji.

### 1.4 Muundo wa Usimamizi na Uendeshaji

Muundo wa usimamizi na uendeshaji wa TAPANET umeundwa ili kuimarisha uwajibikaji, ufanisi, na uratibu ndani ya mtandao wake. Shirika hili linaongozwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka (AGM), ambao hutoa mwelekeo wa kimkakati na mwongozo wa sera. AGM linaundwa na mashirika ya paralegal yaliyosajiliwa kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na ndilo chombo cha juu kabisa cha kufanya maamuzi. Ndilo huchagua Bodi ya Wakurugenzi na kupitisha sera muhimu.

**Mchoro 1: Muundo wa Utendaji**




Bodi ya Wakurugenzi, inayochaguliwa na AGM, hutoa uongozi wa kiutawala na kuhakikisha utekelezaji wa mikakati iliyowekwa. Mratibu wa Kitaifa anaongoza Sekretarieti na kusimamia shughuli za kila siku. Akisaidiwa na vitengo kazi muhimu ambavyo ni: Ufuatiliaji na Tathmini, Utetezi, Ujenzi wa Uwezo, Utafiti na Uchapishaji, pamoja na Fedha na Utawala.

Muundo huu unaiwezesha TAPANET kutekeleza Mpango wake Mkakati kwa ufanisi na kuimarisha nafasi yake katika kupanua upatikanaji wa haki kwa wananchi nchini kote.

### 1.5 Mbinu na Njia zilizotumika Kuandaa Mpango Mkakati huu

Uandishi wa Mpango Mkakati wa TAPANET wa 2025–2029 uliandaliwa kwa kutumia mbinu shirikishi, inayozingatia ushahidi na mashauriano ya wadau, kufuatia kumalizika kwa Mpango Mkakati wa 2020–2024 na hitaji la kuweka mwelekeo mpya kwa mtandao. Mchakato huu uliundwa mahsusi ili kujifunza kutokana na utekelezaji wa mpango uliopita huku ukizingatia mahitaji yanayoendelea kubadilika ya mashirika ya Wasaidizi wa kisheria na mazingira ya upatikanaji wa haki nchini Tanzania kwa ujumla.

Mwongozo wa kazi (Terms of Reference - ToR) ulitungwa ili kuongoza mchakato huu na kuhakikisha mapitio sahihi ya Mkakati uliopita. Mbinu iliyotumika ilijumuisha mchanganyiko wa mbinu za ubora na uchambuzi wa kitaalamu ili kutoa taarifa sahihi na kuweka msingi madhubuti wa mwelekeo wa kimkakati.

**Vipengele muhimu ilikuwa ni pamoja na:**

- **Tathmini ya kina ya Mpango wa 2018–2024** ilifanyika ili kupima utendaji, kubaini mafanikio, changamoto, na mapungufu katika utekelezaji. Tathmini hii ilisaidia katika kuweka maeneo ya kipaumbele na mwelekeo wa taasisi kwa mpango mpya.
- **Mapitio ya nyaraka za sera, mifumo ya kisheria, ripoti, na mikakati ya sekta** mbalimbali yalifanyika ili kuweka nafasi ya TAPANET katika muktadha wa kitaifa na kimataifa wa sekta ya haki.
- **Uainishaji na uchambuzi wa wadau muhimu** ulifanyika, wakiwemo wanachama, taasisi za serikali, wafadhili, na asasi za kiraia. Maoni yao yalikusanywa kupitia mashauriano ili kuhakikisha ushirikishwaji na mpango unaoendana na matarajio ya wadau.
- **Uchambuzi wa mazingira ya ndani na ya nje ya TAPANET** ulifanyika kwa kutumia mbinu za SWOT (Nguvu, Udhaifu, Fursa, Vitisho) na PESTEL (Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii, Kiteknolojia, Kimazingira, Kisheria). Mbinu hizi zilitumika kuelewa kwa kina hatari, fursa, na changamoto za kimfumo zinazoweza kuathiri utekelezaji wa mkakati wa TAPANET.

Matokeo ya mbinu hizi yote yaliunganishwa ili kuunda upya Dira, Dhamira, Maadili ya Msingi, Malengo ya Mkakati, Viashiria vya Utendaji, Mikakati ya Kudhibiti Hatari, na Hatua za Kipaumbele za TAPANET kwa kushirikiana na wanachama, wajumbe wa bodi na sekretariati. Njia zilizotumika kutengeneza mkakati huu zimehakikisha kuwa Mpango Mkakati huu umejengwa juu ya ushahidi, unazingatia sauti za wadau, na unaweza kutekelezwa kwa ufanisi.



# 2. Historia na Mustakabari wa TAPANET

### 2.0. Muktadha na Historia ya TAPANET

### 1. Historia ya TAPANET

TAPANET ilianzishwa mwaka 2007 na kusajiliwa rasmi mwaka 2010 kama mtandao wa mashirika yanayotoa huduma za wasaidizi wa kisheria Tanzania Bara. TAPANET ilianzishwa kabla ya kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria (Legal Aid Act) kwa lengo la kuratibu kazi za wasaidizi wa kisheria. Kabla ya mwaka 2017, kazi za wasaidizi wa kisheria hazikuwa rasmi na hazikufuata mfumo ulioratibiwa. Wasaidizi wa kisheria walifanya kazi katika mazingira yasiyo rasmi, mara nyingi kupitia mashirika ya kijamii au asasi zisizo za kiserikali (NGOs), wakitoa msaada wa kisheria na elimu kwa jamii zilizo pembezoni.

Hata hivyo, kutokuwepo kwa utambuzi rasmi na mwongozo wa kisheria kulileta changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mafunzo ya kina, ukosefu wa ithibati (accreditation), viwango visivyolingana, na kutopata msaa wa kutosha kwa wasaidizi na uratibu holela.

Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 ilijibu changamoto hizi kwa kuitambua rasmi kazi ya wasaidizi wa kisheria, kuweka mfumo wa uthibitisho, na kuanzisha viwango vya mafunzo na uendeshaji. Hatua hii imeongeza kwa kiasi kikubwa ufanisi na upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria nchini Tanzania. Kazi za wasaidizi wa kisheria zinaboresha upatikanaji wa haki kama inavyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kifungu cha 13(1), kinachohakikisha usawa mbele ya sheria na haki sawa ya kisheria kwa wote.

### 2.2. Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017

Sheria hii inatoa mfumo thabiti wa kudhibiti na kuratibu huduma za msaada wa kisheria, kuhakikisha watu wasiojiweza wanapata haki. Sheria inatambua rasmi mchango muhimu wa wasaidizi wa kisheria kama watu waliopata mafunzo na kuthibitishwa kwa ajili ya kutoa msaada wa kisheria.

Wasaidizi wa kisheria husaidia kupunguza gharama za kupata msaada wa kisheria kwa kutoa huduma bila malipo au kwa gharama ndogo, kutoa mwongozo katika masuala ya sheria, na kutetea haki za binadamu. Wanawezesha jamii kwa kuongeza uelewa kuhusu haki na wajibu wa kisheria, pamoja na

kukusanya takwimu kwa ajili ya kuathiri mabadiliko ya sera na sheria.

Kama mtandao wa mashirika ya wasaidizi wa kisheria, TAPANET ina mchango mkubwa katika kuimarisha upatikanaji wa haki katika ngazi ya jamii kupitia wanachama wake. TAPANET hujenga uwezo wa wanachama wake kupitia mafunzo, uhamasishaji wa jamii, na kukuza ushirikiano kati ya wasaidizi wa kisheria na watoa huduma wengine wa msaada wa kisheria. TAPANET pia hutetea mabadiliko ya sera na sheria zinazowanufaisha watu walioko pembezoni, kuhakikisha mfumo wa sheria unakuwa wa haki kwa wote.

### 2.3. Wajibu wa Wasaidizi wa Kisheria Tanzania

Wajibu mkuu wa wasaidizi wa kisheria ni kutoa huduma za msaada wa kisheria, ambazo zinajumuisha elimu na taarifa za kisheria, ushauri wa kisheria, msaada wa kushughulikia kesi, na uwakilishi wa kisheria kwa watu wasiojiweza. Wasaidizi wa kisheria wana nafasi muhimu sana katika kuongeza upatikanaji wa haki kwa kutoa huduma za kisheria bila malipo au kwa gharama nafuu, kuwaongoza wananchi kupitia taratibu za kisheria, na kutetea haki za binadamu.

Wanawezesha jamii kwa kuongeza uelewa kuhusu haki na wajibu wao wa kisheria, na hukusanya takwimu ili kutetea mabadiliko ya sera na sheria. Sheria inahakikisha kwamba wasaidizi wa kisheria wanapata ujuzi na maarifa ya msingi yanayowawezesha kusaidia kikamilifu jamii zilizo pembezoni, hivyo kuziba pengo kati ya mfumo rasmi wa sheria na watu wanaouhitaji zaidi.

Katika eneo la upatanishi na utatuzi wa migogoro, wasaidizi wa kisheria husaidia kutatua migogoro ndani ya jamii kwa kupatanisha pande zinazohusika na kuwezesha maafikiano ya amani. Wanaendeleza na kusaidia matumizi ya mbinu mbadala za utatuzi wa migogoro ili kuepusha kesi kuchukua muda mrefu mahakamani, hivyo kufanya haki kuwa rahisi na ya haraka kupatikana.

Mbali na jukumu lao kuu la kuelimisha jamii na kuwawezesha kisheria, wasaidizi wa kisheria pia wanahusika katika kazi za uchechemuzi na ushawishi wa sera. Kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za serikali, wanashughulikia changamoto za kimfumo na kusaidia maendeleo ya jamii. Kwa njia hiyo, wanatetea mabadiliko ya sheria yanayoboreshwa upatikanaji wa haki na kulinda haki za binadamu. Mtandao na ushirikiano ni vipengele muhimu katika kazi ya msaidizi wa kisheria. Wanashirikiana na wataalamu wa sheria kama wanasheria na majaji ili kuhakikisha msaada wa kisheria unafikiwa kwa ufanisi. Pia hujenga na kudumisha mitandao ndani ya jamii ili kuimarisha msaada na upatikanaji wa haki.

Kwa ujumla, wasaidizi wa kisheria ni sehemu muhimu ya mfumo wa sheria wa Tanzania, wakitoa msaada wa msingi na kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa kila raia. Majukumu yao mbalimbali yanawafanya kuwa wahusika wa lazima katika kuunganisha taasisi rasmi za sheria na jamii wanazozihudumia.

Katika kuhakikisha wanachama wake wanatimiza majukumu yao ipasavyo, TAPANET ina nafasi muhimu ya kuunga mkono mashirika wanachama kwa kuendeleza ushirikiano baina ya wasaidizi wa kisheria na watoa huduma wengine wa msaada wa kisheria. TAPANET hutangaza mbinu bora na kushiriki rasilimali, hivyo kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za kisheria.

Aidha, TAPANET hutoa uratibu na msaada kwa wanachama wake ili kuwasaidia kushughulikia changamoto za kisheria na urasimu zinazoweza kuwazuia kufanya kazi zao kwa ufanisi. Mbinu hii ya ushirikiano na msaada huimarisha kwa kiasi kikubwa athari ya kazi za wasaidizi wa kisheria katika ngazi ya jamii.

## 2.4. Changamoto Zinazokabili TAPANET

Licha ya kuwa na athari kubwa, TAPANET inakutana na changamoto kadhaa ambazo zinahitaji mpango mpya wa kimkakati:

i. Mfumo wa Kisheria na Utawala: Kushughulikia mazingira ya kisheria na utawala ambayo ni changamoto na inahitaji rasilimali nyingi. Changamoto hii inahitaji mbinu rahisi za kusimamia majukumu ya utawala kwa ufanisi.
ii. Ujenzi wa Uwezo: Hakikisha kwamba mashirika yote wanachama yana ufanisi wa kutosha na ujuzi wa kimafunzo ni changamoto kubwa. Ujenzi wa uwezo unahitaji rasilimali kubwa na utaalamu, ambayo inaonyesha umuhimu wa kuwa na programu imara za mafunzo na mifumo ya msaada.
iii. Uratibu na Ushirikiano: Ufanisi katika uratibu na ushirikiano kati ya mashirika mbalimbali wanachama unahitaji mawasiliano na muelekeo wa pamoja. Kufanikisha mwelekeo huu kunaweza kuwa changamoto lakini ni muhimu kwa mafanikio ya mtandao.
iv. Ushirikiano na Jamii: Kuhusisha na kuhamasisha jamii kwa kiwango kikubwa ni muhimu kwa mashirika yanayoendeshwa na TAPANET, ambayo hutegemea wanachama wake kuendesha ushiriki wa jamii na kuimarisha uaminifu. Hii inahitaji juhudi endelevu na rasilimali ili kuhakikisha ushiriki mzuri katika maeneo mbalimbali.
v. Ufuatiliaji na Tathmini: Kutekeleza mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini ya athari ya jitihada za pamoja ni muhimu lakini inahitaji rasilimali nyingi. TAPANET inakutana na changamoto za kukusanya takwimu na kupima athari ya juhudi zake kutokana na mifumo dhaifu ya ufuatiliaji na tathmini. Balancing mahitaji ya wafadhili na mbinu za ufanisi ni changamoto kubwa.

vi. Mazingira ya Kisiasa: Mazingira ya kisiasa yanatoa changamoto, hasa kwa wale wanaoshiriki katika kazi za uchechemuzi. Inahitajika mbinu ya kujali mazingira ya kisiasa ili kufanikisha malengo ya TAPANET.

vii. Ushirikiano wa Wanachama: Kuendelea kuhamasisha na kudumisha ushiriki wa wanachama kutoka mashirika mbalimbali ni changamoto kutokana na maslahi na vipaumbele mbalimbali. Vizuizi vya mawasiliano, upungufu wa rasilimali, na kudumisha motisha kwa muda mrefu vinazorotesha juhudi za ushirikiano.

Mafunzo muhimu yaliyopatikana kutokana na mpango mkakati uliopita ni pamoja na umuhimu wa kuwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini (M&E) unaoongozwa na takwimu, hitaji la kujitegemea kifedha, na changamoto ya kuratibu mtandao mkubwa na wenye utofauti wa wanachama. Maarifa haya yalisaidia kuunda malengo ya kimkakati yaliyo bora zaidi na yanayoelekezwa kwenye matokeo kwa kipindi cha 2025–2029.

Kwa muhtasari, utekelezaji wa mpango mkakati uliopita ulibainisha mapungufu katika maeneo yafuatayo:

- Ushiriki wa wanachama,
- Ujumuishaji wa mifumo ya kidijitali,
- Uhamasishaji wa rasilimali, na
- Ushawishi wa sera.

Mafunzo haya sasa yanakuwa msingi wa mpango wa sasa wa TAPANET, ambao unachukua mtazamo ulio na muundo thabiti zaidi, unaolenga uendelevu na unaoongozwa na ushahidi.

Changamoto zilizotajwa hapo juu zinathibitisha haja ya kuwa na mpango mpya wa kimkakati wa TAPANET ambao utaongoza mtandao huu kuelekea kutimiza dira yake huku ukitekeleza dhamira yake.

## 2.5. **Uchambuzi wa Mazingira** (SWOT & PESTEL)


Ili kuelewa kwa kina hali ya sasa ya kimkakati ya TAPANET na kubaini maeneo ya kuboresha, wanachama walifanya uchambuzi wa Kina kujuwa Nguvu ya TAPANET, udhahifu, fursa na mambo hatarishi (SWOT Analysis). Uchambuzi huu ulizingatia mazingira ya ndani na ya nje yanayoathiri mwelekeo wa TAPANET.

Pia, uchambuzi huu uihusisha kuangalia mambo ya nje kwa kutumia njia ya PESTEL analysis ambao iliangazia uchambuzi wa mazingira ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiteknolojia, kisheria, na kimazingira yana athari kubwa kwa operesheni za TAPANET.

- **Kisiasa**: TAPANET inahitaji kushughulikia changamoto za uchechemuzi wa sera wakati ikitumia ushirikiano wa serikali ili kuboresha mifumo ya msaada wa kisheria.

- **Kiuchumi**: Upungufu wa rasilimali na utegemezi wa wafadhili ni hatari, ikihitaji juhudi kubwa za kukusanya rasilimali.
- **Kijamii**: Uhitaji mkubwa wa huduma za msaada wa kisheria, hasa kwa makundi yaliyosahaulika, unatoa changamoto na fursa kwa TAPANET kupanua ushiriki na utoaji wa huduma.
- **Kiteknolojia**: Mabadiliko ya kidijitali yanaweza kuboresha ufanisi, lakini yanahitaji uwekezaji katika kupitisha ICT na mifumo ya huduma za kisheria za kidijitali.
- **Kisheria**: Sheria za kiutawala na urasimu zinazuia utoaji wa huduma, wakati changamoto za mabadiliko ya kisera zinahitaji jitihada za uchechemuzi.
- **Kimazingira**: Mabadiliko ya tabianchi na majanga yanazidisha mahitaji ya msaada wa kisheria, wakati vikwazo vya kisheria kama vile ucheleweshaji wa taratibu na vizuizi vya udhibiti vinaathiri utoaji wa huduma

**Mchoro 2: Uchambuzi maswala ya nje (PESTEL)**




Kwa upande wa ndani, TAPANET inanufaika na mtandao mpana wa kijiografia, sekretarieti inayofanya kazi kwa ufanisi, na uhusiano mzuri na wadau, wakiwemo wadau wa serikali. Hata hivyo, kuna udhaifu unaohitaji kushughulikiwa ikiwa ni pamoja na changamoto za kifedha, utegemezi mkubwa kwa wafadhili, mapungufu ya mawasiliano, na changamoto katika utekelezaji wa miradi.

Kwa upande wa nje, fursa zipo katika mahitaji makubwa ya msaada wa kisheria, nafasi ya kushawishi sera, na mabadiliko ya kidijitali. Hata hivyo, kuna vitisho kama mabadiliko ya vipaumbele vya wafadhili, ushindani mkali wa kupata fedha, na kushuka kwa ushiriki wa wanachama, ambavyo vinahitaji kushughulikiwa kupitia mipango ya kimkakati na ushirikiano wa wadau.

Kwa kutumia vizuri nguvu na fursa zilizopo huku ikikabili udhaifu na vitisho vilivyopo, TAPANET inaweza kuboresha utoaji wa huduma za msaada wa kisheria, juhudi za uchechemuzi wa sera, na uendelevu wa shirika kwa ujumla.

**Mchoro 3: Uchambuzi wa Mambo ya ndani**




## 2.4 Uchambuzi wa Wadau (Stakeholder Analysis)

Wadau, wahusika wakuu, wapinzani, mashujaa, na wenye ushawishi—hata kama lugha inatofautiana, wote wanarejelea hitaji la kushirikiana na makundi mbalimbali yanayohusika katika upatikanaji wa haki.

Hivyo basi, aina ya wadau ambao TAPANET inapaswa kushirikiana nao ni wale walioteuliwa kwa makini na mtandao. Sehemu hii inahusu uchambuzi wa wadau ambao motisha zao zinaendana na dhamira na maono ya TAPANET.

### 2.4.1. Aina ya Wadau

Wadau mbalimbali wameainishwa kushirikiana na TAPANET, kuanzia ngazi ya juu hadi chini. Katika ngazi ya juu tunajumuisha wizara, kamati za bunge, na taasisi za serikali. Hawa ni pamoja na:

- *Wanaounga mkono na wenye ushawishi*
- *Wafaidika*
- *Wasio waungaji mkono*

Katika ngazi ya chini, yapo mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanayofanya kazi za msaada wa kisheria, pamoja na viongozi wa dini, viongozi wa jadi, na viongozi wa jamii. Hawa wote ni wadau wenye maslahi, malengo, na mikakati mbalimbali ya utekelezaji, lakini yanayoendana na vipaumbele vya TAPANET.

i. Vigezo vya Uchaguzi wa Wadau:
ii. Ufanisi wa utendaji– Wadau wanaotoa mchango wa moja kwa moja kwa matokeo ya TAPANET, hasa katika maeneo ambayo TAPANET haina uwezo mkubwa wa kufikia.
iii. Ufanisi wa gharama – Wadau ambao ushiriki wao utawezesha utekelezaji wa shughuli za TAPANET kwa gharama nafuu.
iv. Uhusiano wa moja kwa moja na TAPANET – Wadau ambao malengo na kazi zao zinaendana na maono na kazi za TAPANET.
v. Uendelevu – Matokeo yatakayofikiwa kupitia TAPANET yataendelezwa kupitia ushirikiano wa wadau husika.
vi. Maadili – Wadau ambao wanafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria na viwango vya kimataifa na kitaifa vya haki za binadamu.
vii. Utekelezekaji – Pale ambapo kuna suala muhimu linalohitaji ushirikishwaji wa mdau fulani, ama kujibu changamoto za nje, au kutafuta njia mpya za kuboresha au kupanua uingiliaji.

### 2.4.2. Wadau Wakuu wa TAPANET

Kulingana na uchambuzi wa wadau uliofanyika, TAPANET inashirikiana na taasisi za serikali, wafadhili, mashirika ya kiraia, taasisi za sheria, na vyombo vya habari ili kuimarisha msaada wa kisheria,

kuongeza uchechemuzi wa sera, na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa haki.

Jedwali: Wadau na Mikakati ya Ushirikiano

| Mdau | Wajibu | Kiwango cha Maslahi | Mikakati ya Ushirikiano |
|---|---|---|---|
| MoCLA (Wizara ya Katiba na Sheria) | Kusimamia na kusaidia sekta ya wasaidizi wa kisheria | Juu | Majadiliano ya sera, mipango ya pamoja |
| Mahakama | Kusimamia mfumo wa sheria na utatuzi wa migogoro (ADR) | Wastani | Mafunzo ya pamoja, ushirikiano kwenye huduma za mahakama |
| Vyombo vya habari | Kuongeza uelewa na elimu kwa umma | Wastani | Kampeni za elimu ya sheria, ushirikiano katika habari |
| Wafadhili – DANIDA, EU, LSF, n.k. | Kufadhili shughuli za TAPANET na msaada wa kisheria | Juu | Uwasilishaji wa taarifa za kifedha na athari kwa uwazi |
| CSOs/NGOs | Kufikia jamii, kutoa msaada wa kisheria | Juu | Majukwaa ya pamoja, utetezi wa pamoja |
| Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) | Utekelezaji wa sheria ngazi ya wilaya | Juu | Ujenzi wa uwezo, mizunguko ya maoni kutoka kwa jamii |
| Washirika wa Maendeleo | Kutoa msaada wa kitaalamu na sera | Wastani | Mipango ya pamoja, ushirikiano wa ushahidi na ufuatiliaji |

## 2.5. Huduma Zinazotolewa na Wanachama wa TAPANET

Mashirika wanachama wa TAPANET yanatoa huduma mbalimbali kama vile elimu ya kisheria, upatanishi wa migogoro, msaada wa uangalizi wa watoto, ushauri kuhusu ardhi na mali, na msaada kwa manusura wa ukatili wa kijinsia. Huduma hizi ni muhimu sana katika kuboresha upatikanaji wa haki katika ngazi ya jamii.

Mashirika haya ya wasaidizi wa kisheria pia yanalenga kuelimisha jamii kuhusu haki zao za kisheria, kutoa elimu ya uraia, kuongeza uelewa kuhusu haki za binadamu, kutoa ushauri wa kisheria na kushughulikia changamoto nyingine zinazowakumba wanajamii.

Programu endelevu za elimu ya msaada wa kisheria na uhamasishaji ni muhimu kwa kuwaelimisha wananchi kuhusu haki zao, taratibu za mahakama, usuluhishi, mfumo wa haki jinai, na mbinu mbadala za utatuzi wa migogoro (ADR). Hata hivyo, wanachama wa TAPANET wanakabiliwa na changamoto kubwa za uratibu na kuhakikisha ubora wa huduma wanazotoa.

Ingawa vituo vya wasaidizi wa kisheria vipo katika wilaya zote za Tanzania, TAPANET na wanachama wake wanakumbwa na changamoto za uwezo, hali inayosababisha pengo la maarifa na upatikanaji mdogo wa programu za mafunzo, rasilimali za kisheria, ufadhili, na fursa za maendeleo ya kitaaluma. Aidha, ushiriki wa wanachama katika kuboresha huduma za msaada wa kisheria bado ni changamoto inayohitaji kushughulikiwa.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, TAPANET inapanga kuandaa warsha na semina za mafunzo mara kwa mara—kwa njia ya ana kwa ana na mtandaoni—kuongeza vyanzo vya rasilimali na kutumia majukwaa ya kidijitali. Kuanzisha programu za ushauri kati ya wanasheria wakongwe na wasaidizi wa kisheria wapya pia kutakuwa na manufaa.

Zaidi ya hayo, ushirikiano na taasisi za sheria, mashirika ya serikali na NGOs unaweza kutoa msaada na ufadhili wa kukuza uwezo. Ushirikiano wa jamii kupitia programu za uhamasishaji na mifumo ya kutoa mrejesho ni muhimu kuhakikisha kuwa huduma za msaada wa kisheria zinakidhi mahitaji ya jamii.

Kwa kutekeleza suluhisho hizi, TAPANET itaongeza uwezo wa wasaidizi wa kisheria na kuhakikisha wanatoa msaada wa kisheria ulio bora na jumuishi kwa jamii zilizo pembezoni. Hatua hizi zitasaidia kuwawezesha wananchi kutumia haki zao za kisheria na kupata haki. Juhudi hizi zote ndizo msingi wa haja ya kuwa na mkakati mpya wa TAPANET.

.

# 3. Malengo na Vipaumbele Vyetu



### 3.0. Vipaumbele, Malengo na Mikakati ya Mwaka 2025–2029

Mpango Mkakati huu wa TAPANET 2025–2029 umeundwa ili kuelekeza juhudi za TAPANET katika kujenga mtandao endelevu na wenye uwezo wa mashirika ya wasaidizi wa kisheria kote Tanzania. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, mfumo huu utatumika kama ramani ya njia ya kuongeza upatikanaji wa haki kwa jamii zilizo pembezoni.

Kwa kulenga malengo makuu kama vile kupanua uanachama wa TAPANET, kutetea mazingira bora ya kazi, kuwawezesha mashirika ya wasaidizi wa kisheria, kuimarisha muundo wa shirika la TAPANET, na kuhamasisha ushiriki wa wanachama—TAPANET inalenga kuhakikisha utawala bora, uratibu madhubuti, na huduma bora za msaada wa kisheria.

Dhamira ya TAPANET ya kujifunza kila mara na kusaidia jamii itaongoza mtandao huu kufikia lengo lake la kuwawezesha na kudumisha kazi ya wasaidizi wa kisheria nchini Tanzania, hatimaye kuwezesha jamii kutumia haki zao na kupata haki..

Sehemu ifuatayo imeainisha dira, dhamira na lengo kuu la TAPANET. Pia imeelezea maeneo manne ya kipaumbele na kimkakati ambayo TAPANET itayazingatia katika kipindi cha miaka mitano.


**Mchoro 4:Dira, Dhamira na lengo**




### 3.1 Nadharia Yetu ya Mabadiliko (Theory of Change)

***Iwapo TAPANET itaongeza uwezo na taaluma kwa wasaidizi wa kisheria, itatetea mageuzi ya kisheria na kisera, itahakikisha uendelevu wa kifedha, na kupanua ushiriki wa wanachama, basi mtandao madhubuti na ulio tayari kuhudumia jamii utaibuka. Matokeo yake ni: Wasaidizi wa kisheria wataweza kutoa huduma bora zaidi; Jamii zilizo pembezoni zitapata haki kwa urahisi zaidi; Kutatokea ongezeko la utambuzi wa kisheria na ufadhili wa msaada wa kisheria; Hatimaye, kutakuwa na mageuzi ya mfumo wa sheria, haki jumuishi zaidi, na uwezeshaji wa kisheria kwa makundi yaliyo pembezoni kote Tanzania***.

**Mchoro 5: Nadharia ya mabadiriko (ToC)**




Nadharia hii ya mabadiliko inategemea msingi kwamba utambuzi wa kisheria, uchechemuzi unaotegemea takwimu, na ushirikiano endelevu wa wanachama utaleta athari za kimfumo. Njia yetu ni shirikishi, inayojifunza kwa kutenda, na inayojibadilisha kulingana na hali halisi.

### 3.1. Maelezo ya Malengo na Maeneo ya Kipaumbele ya Mkakati

Maeneo ya Kipaumbele ya Kimkakati yaliyoainishwa hapa chini yanawakilisha msingi wa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa TAPANET. Maeneo haya yanajikita katika kuimarisha uwezo, uratibu, na ufanisi wa mtandao wa wasaidizi wa kisheria ili kutoa huduma jumuishi na bora za msaada wa kisheria kwa jamii zisizohudumiwa ipasavyo kote Tanzania.


Kwa kulenga maeneo haya muhimu, TAPANET inalenga kuunda mtandao endelevu na wenye uwezo wa mashirika ya wasaidizi wa kisheria ambao wanaweza kushughulikia mahitaji mbalimbali ya kisheria ya jamii, kukuza haki, na kuhakikisha kuwa kila mtu anapata haki zake za kisheria.

Kila eneo la kimkakati linajumuisha hatua mahususi na matokeo yanayotarajiwa ambayo yanaendana

na dira na dhamira ya TAPANET, na hivyo kuongoza juhudi zake kuelekea jamii yenye haki na usawa zaidi.

.

**Mchoro 6: Vipaumbele vya Mpango Mkakati**




### 3.1.1 Kipaumbele cha kwanza: Utaalamu na Taaluma

**Lengo la Mkakati wa kwanza**: Kuimarisha uwezo na taaluma ya wasaidizi wa kisheria ili kuongeza upatikanaji wa haki

Wasaidizi wa kisheria hufanya kazi katika mazingira yenye uhaba wa rasilimali, wakiwa hawana mafunzo maalum, mifumo ya maadili ya kitaaluma, wala mifumo sanifu ya utoaji huduma. Kukosekana kwa njia rasmi ya ukuaji wa taaluma pamoja na mfumo wa uthibitisho huathiri ubora na uaminifu wa kazi zao.
Kuimarisha uwezo wa wasaidizi wa kisheria kutasaidia kuziba pengo lililopo kati ya wataalamu wa sheria na jamii zisizohudumiwa ipasavyo, na hivyo kuhakikisha kuwa watu wote wanapata haki bila kujali hali yao ya kiuchumi.

**Lengo la Kimkakati #1:** Kuimarisha uwezo na taaluma ya mashirika ya wasaidizi wa kisheria ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora za msaada wa kisheria.

*Mikakati ya kutekeleza lengo la 1:*

- Ujenzi wa uwezo na maendeleo ya kitaaluma: Kutoa mafunzo maalum kuhusu msaada wa kisheria, haki za binadamu, usawa wa kijinsia, haki za ardhi, na ulinzi wa watoto.

- Kuimarisha taasisi za wasaidizi wa kisheria: Kutoa mafunzo kuhusu utawala bora, usimamizi wa fedha, na uundaji wa sera, sambamba na kusaidia usajili wa kisheria na ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria.

- Kuboresha matumizi ya teknolojia na usaidizi wa kidijitali: Kutoa mifumo ya usimamizi wa kesi kwa njia ya kidijitali, kuwafundisha wasaidizi wa kisheria ukusanyaji wa takwimu, na kukuza mashauriano ya kisheria kwa njia ya mtandao.

- Utambuzi na ushirikiano na wadau: Kuimarisha ushirikiano na taasisi za serikali, kuanzisha Siku Maalum ya TAPANET kila mwaka, na kukuza ushiriki wa wasaidizi wa kisheria katika majukwaa ya haki kitaifa na kikanda.

- Usanifishaji na uthibitisho: Kuandaa mfumo wa kitaifa wa uthibitisho wa wasaidizi wa kisheria ili kuhakikisha viwango vya taaluma na utoaji huduma vinakuwa sanifu.

- Mafunzo kwa njia ya ushauri na ujifunzaji rika: Kuweka programu za ushauri kati ya wasaidizi wenye uzoefu na wale wapya ili kuwezesha ubadilishanaji wa ujuzi.

- Elimu ya sheria kwa jamii: Kuwafundisha wasaidizi wa kisheria kuendesha warsha za uelewa wa sheria na kampeni za uhamasishaji katika jamii zisizohudumiwa ipasavyo.

- Mfumo wa ukuaji wa taaluma ya wasaidizi wa kisheria: Kuandaa njia rasmi za ukuaji wa kazi, motisha, na programu za mafunzo endelevu kwa ajili ya kitaaluma ya huduma za msaada wa kisheria.

Kupitia Lengo la Kwanza la Kimkakati, TAPANET inalenga kujenga mtandao thabiti na wenye usaidizi wa wasaidizi wa kisheria unaoweza kushughulikia mahitaji ya kisheria katika ngazi ya jamii. Ujenzi wa uwezo na kuwawezesha wanachama kutahakikisha kuwa mashirika wanachama wa TAPANET yamejiandaa kikamilifu kutoa huduma za msaada wa kisheria zenye athari na kushiriki kikamilifu katika kutimiza dhamira ya kuongeza upatikanaji wa haki nchini Tanzania.

Lengo hili la kimkakati ni msingi muhimu katika kujenga mtandao imara, endelevu, na wenye uwezo, unaoweza kuchochea mabadiliko chanya ya kijamii

### 3.1.1. Kipaumbele cha Pili: uchechemuzi na Maendeleo ya Sera

**Lengo la Mkakati 2**: Kutetea mazingira wezeshi ya kisheria na kisera kwa ajili ya huduma endelevu za msaada wa kisheria.

Wasaidizi wa kisheria hufanya kazi katika mazingira tata na yenye vikwazo vya kisheria. Baadhi ya mifumo ya sasa ya sheria haizingatii ipasavyo huduma za msaada wa kisheria zinazotolewa katika ngazi ya jamii, jambo ambalo hupunguza uwezo wa wasaidizi wa kisheria kuwahudumia wanaohitaji msaada huo.

Aidha, kuna ukosefu wa fedha mahsusi kwa ajili ya mashirika ya wasaidizi wa kisheria, hali inayopunguza uwezo wao wa kufanya kazi kwa ufanisi. Kuimarisha mfumo wa sera na kutambuliwa rasmi kwa wasaidizi wa kisheria katika taasisi za sheria kutasaidia kujenga mfumo wa haki jumuishi na endelevu—hasa kwa wanawake, watoto, na makundi yaliyotengwa yanayohitaji msaada wa kisheria unaolengwa mahususi.

**Lengo la Kimkakati #2:** Kuhakikisha mazingira wezeshi ya kisheria na kisera yanayoboreshwa upatikanaji wa haki na kuimarisha mashirika ya wasaidizi wa kisheria.

*Mikakati ya kutekeleza lengo la 2:*

- **i.** Utambuzi wa kisheria na mageuzi ya sera: Kutetea utambuzi rasmi wa wasaidizi wa kisheria katika mahakama, vituo vya polisi, na mifumo ya utawala, sambamba na kushinikiza mabadiliko ya sera na sheria.
- **ii.** uchechemuzi wa haki za binadamu na haki za kijinsia: Kuanzisha kliniki maalum za msaada wa kisheria kwa manusura wa ukatili wa kijinsia (GBV), kuhakikisha ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu (PWDS), na kuwapa mafunzo wasaidizi wa kisheria kuhusu kushughulikia kesi za ardhi na jinsia.
- **iii.** Uwezeshaji wa kisheria unaoongozwa na jamii: Kuendesha kampeni za uhamasishaji wa umma, kuimarisha ushirikiano na asasi za kiraia (CSOs), na kuandaa nyenzo za elimu ya sheria kwa lugha za kienyeji.
- **iv.** Ufuatiliaji na uchechemuzi unaotegemea takwimu: Kuanzisha mfumo wa taarifa wa wakati halisi

wa ukiukwaji wa haki za binadamu, kutumia takwimu kwa uchechemuzi wa sera, na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

- **v.** Ushirikiano wa wadau mbalimbali: Kuwezesha majadiliano kati ya serikali, asasi za kiraia, na sekta binafsi ili kuongeza uungwaji mkono wa sera zinazosaidia huduma za msaada wa kisheria.
- **vi.** Ujumuishaji katika mfumo wa mahakama: Kushirikiana na vyombo vya mahakama kuwaingiza wasaidizi wa kisheria katika mifumo ya utatuzi mbadala wa migogoro (ADR) na huduma za msaada ndani ya mahakama.
- **vii.** uchechemuzi wa mfuko wa ruzuku wa msaada wa kisheria: Kushirikisha taasisi za serikali na washirika wa maendeleo kuanzisha mfuko wa kitaifa kwa ajili ya huduma za wasaidizi wa kisheria.
- **viii.** Vyombo vya habari na kampeni za uhamasishaji: Kutumia majukwaa ya vyombo vya habari kutangaza sera za msaada wa kisheria, kutoa nafasi kwa sauti za makundi yaliyo pembezoni, na kuonyesha umuhimu wa msaada wa kisheria unaotolewa kwa jamii..

**Lengo hili la kimkakati la pili** litaiwezesha TAPANET kuchangia katika kujenga jamii yenye haki na usawa, ambako kila mtu—hasa wale walioko pembezoni—wanaweza kutumia haki zao za kisheria na kupata haki kwa usawa. Eneo hili la kimkakati ni muhimu sana katika kushughulikia changamoto za kimfumo na kuhakikisha kuwa huduma za msaada wa kisheria zinazotolewa na TAPANET na wanachama wake ni bora na endelevu.

### 3.1.2. Kipaumbele cha 3: Uendelevu wa Shirika

**Lengo la Mkakati #3**: Kuhakikisha uendelevu wa TAPANET na ufanisi wa utoaji hudumavkutoka kwa wanachama wake

TAPANET na mashirika yake wanachama wanakabiliwa na changamoto za uendelevu wa kiutendaji na kifedha. Utegemezi mkubwa wa mashirika mengi ya wasaidizi wa kisheria kwa mfadhili mmoja hupunguza uwezo wa kupanga kwa mkakati wa muda mrefu, huku miundombinu dhaifu ya utawala wa ndani ikiathiri mchakato wa kufanya maamuzi na uwajibikaji.

Kuimarisha utawala wa taasisi, kubuni vyanzo mbalimbali vya rasilimali, na kuboresha utoaji wa huduma ni mambo ya msingi ili kuhakikisha TAPANET inabaki kuwa shirika lenye ufanisi na uhuru. Aidha, kuwa na wanachama walio imara na wanaoshiriki kikamilifu ni jambo muhimu kwa uendelevu wa TAPANET na mafanikio ya shughuli zake za uchechemuzi. Kuimarisha uhifadhi wa wanachama, usajili wa wanachama wapya, na ushiriki wao katika shughuli za mtandao kutahakikisha mtandao madhubuti na wenye nguvu wa wasaidizi wa kisheria.

**Lengo la Kimkakati 3.1:** Kuimarisha utawala wa taasisi ya TAPANET, uendelevu wa kifedha, na utoaji wa huduma.

*Mikakati ya kutekeleza lengo la 3.1*:

- Kuimarisha utawala na usimamizi: Kuendeleza uongozi kupitia maboresho ya bodi, uwazi wa kifedha, na upangaji mkakati.
- Kubuni vyanzo mbalimbali vya uendelevu wa kifedha: Kukuza mifumo ya uchangishaji wa rasilimali katika ngazi ya ndani, kuanzisha shughuli za uzalishaji wa mapato, na kuimarisha ushirikiano na serikali, sekta binafsi, na mashirika ya maendeleo.
- Kupanua huduma za msaada wa kisheria zinazoongozwa na jamii: Kuanzisha kliniki za msaada wa kisheria zinazotembea, kutumia teknolojia ya kidijitali kwa ajili ya mashauriano, na kuweka mifumo ya mrejesho kwa ajili ya kuboresha huduma.
- Kuimarisha mitandao na ushirikiano wa maarifa: Kuwezesha majukwaa ya msaada wa kisheria ya kikanda na kitaifa, kukuza ubadilishanaji wa uzoefu, na kushiriki katika mipango ya ushirikiano wa mipakani kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kisheria.
- Ufanisi wa kiutendaji na Ufuatiliaji & Tathmini (M&E): Kutekeleza mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya kupima athari na kusaidia maamuzi ya kimkakati.
- Ujenzi wa uwezo kwa uongozi: Kuandaa programu za mafunzo kwa ajili ya viongozi wa TAPANET ili kuboresha utawala, uhamasishaji wa rasilimali, na ushiriki wa wanachama.
- Kuongeza ushiriki wa wanachama: Kuandaa mbinu yenye muundo kwa ajili ya kuongeza ushiriki wa wanachama, kufufua wanachama waliolala, na kukuza uongozi ndani ya mtandao.
- Utoaji wa huduma kwa kutumia teknolojia: Kuwekeza katika majukwaa ya kidijitali ya msaada wa kisheria ili kuboresha ufuatiliaji wa kesi, mawasiliano, na uhamasishaji kwa jamii.
- Viwango vya ubora wa huduma: Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa viwango vya utoaji huduma katika mashirika yote wanachama wa TAPANET ili kuhakikisha uwiano na uwajibikaji.
- Mkakati wa Ushirikiano kati ya Umma na Sekta Binafsi (PPP): Kuwahusisha wadau wa sekta binafsi, programu za uwajibikaji kwa jamii (CSR), na kampuni za sheria kusaidia juhudi za uendelevu.

- Kuimarisha taswira ya TAPANET kwa umma: Kupitia ushirikiano na vyombo vya habari, kusimulia mafanikio ya wanachama, kutengeneza maudhui ya kidijitali, na kutumia simulizi zinazoongozwa na jamii. Mpango wa kuonekana hadharani utaandaliwa ili kuiweka TAPANET kama kinara wa haki za msingi ngazi ya jamii. TAPANET pia itatafuta utambulisho mpya wa kuona, zana za simulizi, na matumizi ya majukwaa kama Twitter, YouTube, na redio za jamii.

- Kuanzisha jukwaa la ushiriki wa wanachama kila robo mwaka na kujaribu tuzo za ubunifu ili kuonyesha kazi bora za msaada wa kisheria. Mfumo wa ushauri (mentorship), zana zinazotengenezwa na wanachama, na ubadilishanaji wa maarifa baina ya wanachama vitaimarishwa. Dashibodi ya kidijitali ya wanachama itawaruhusu kushiriki taarifa, kutoa mrejesho, na kubadilishana maarifa kwa wakati halisi.

**Lengo la Kimkakati 3.2:** Kupanua na kuimarisha msingi wa wanachama wa TAPANET ili kuongeza ushirikiano, ushiriki, na uendelevu wa mtandao.

*Mikakati ya kutekeleza lengo la 3.2:*

- Kampeni maalum za usajili wa wanachama wapya: Kusajili kwa lengo mashirika mapya ya wasaidizi wa kisheria ili kupanua wigo wa TAPANET nchini.
- Programu za mapokezi na utambulisho kwa wanachama wapya: Kuhakikisha wanachama wapya wanaelewa dira, dhamira na fursa za ushiriki ndani ya TAPANET.
- Mikakati ya uhifadhi na uhamasishaji wa wanachama waliolala: Kushughulikia changamoto za kuacha uanachama kwa kubaini sababu kuu na kuweka mifumo ya msaada.
- Maendeleo ya kitaaluma kwa wanachama: Kutoa mafunzo, ushauri (mentorship), na msaada wa ukuaji wa kitaaluma kwa wanachama.
- Utambuzi na motisha: Kuandaa tuzo na motisha ili kuhimiza ushiriki hai wa wanachama.
- Mifumo ya maoni: Kuweka mifumo ya maoni iliyo na muundo thabiti kwa ajili ya kushughulikia mahitaji na changamoto za wanachama.

### 3.2 Usimamizi wa Viashiria Hatarishi (Risk Management)

Usimamizi madhubuti wa viashiria vya hatari ni muhimu kwa mafanikio na uendelevu wa Mpango Mkakati wa TAPANET 2025–2029. Kama mtandao wa kitaifa wa wasaidizi wa kisheria unaofanya kazi katika mazingira ya kisiasa, kisheria, na kifedha yanayobadilika, TAPANET lazima itambue mapema na kushughulikia viashiria vinavyoweza kuhatarisha utekelezaji wa vipaumbele vyake.
Mpango huu wa kimkakati umetumia mfumo mpana wa usimamizi wa hatari hizi, unaogawanya hatari za ndani na nje, kutathmini athari zake, na kupendekeza mikakati ya kupunguza athari hizo. Kwa kuunganisha njia za kukabiliana na hatari katika utekelezaji wa mkakati, TAPANET itaimarisha uhimilivu wake, uwezo wa kujifunza na kubadilika, na kuhakikisha haki kwa jamii inapatikana kwa njia endelevu.

**Jedwari 1; Usimamizi wa Viashiria Hatarishi (Risks)**

| Na. | Hatari | Maelezo | Kiwango cha Athari | Mikakati ya Kukabiliana |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mabadiliko ya kisiasa | Mabadiliko ya sheria, ushawishi wa kisiasa, au mwelekeo wa sera | Wastani | Kuimarisha uhusiano wa kisera, kufuatilia sera kwa karibu, na kubadilika haraka |
| 2 | Ushirikiano wa serikali | Kukosekana kwa msaada au kutotambuliwa rasmi kwa wasaidizi wa kisheria | Juu | Kuanzisha ushirikiano wa kisheria na wizara husika, kutumia takwimu kuathiri maamuzi |
| 3 | Kuchoshwa kwa wafadhili | Kupungua au kusitishwa kwa ufadhili kutokana na mabadiliko ya vipaumbele | Juu | Kubuni vyanzo mbalimbali vya fedha, kuimarisha mikakati ya ufadhili wa ndani |
| 4 | Changamoto za mfumo wa sheria | Kukosekana kwa utambuzi rasmi wa wasaidizi wa | Juu | Kutetea mageuzi ya sera, kushirikiana na wataalamu wa sheria, |

| Na. | Hatari | Maelezo | Kiwango cha Athari | Mikakati ya Kukabiliana |
|---|---|---|---|---|
| | | kisheria | | kuelimisha jamii |
| 5 | Upungufu wa rasilimali | Ukosefu wa fedha kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa uwezo na utawala | Juu | Kuanzisha shughuli za uzalishaji mapato, kuboresha matumizi ya bajeti |
| 6 | Ukosefu wa imani kwa jamii | Uelewa mdogo au kutokuaminiana katika jamii mpya | Wastani | Kampeni za uhamasishaji, kushirikisha viongozi wa jamii, kusimulia mafanikio |
| 7 | Vizuizi vya lugha | Taarifa nyingi za kisheria zikiwa kwa Kiingereza pekee | Wastani | Kutafsiri nyenzo kwa Kiswahili na lugha za wenyeji, warsha za jamii |
| 8 | Udhaifu wa kiutawala | Miundo dhaifu ya ndani na kutokuwepo kwa uwajibikaji wa ndani | Wastani | Kufanyia marekebisho miundo, kuweka taratibu wazi na usimamizi wa utendaji |
| 9 | Ushiriki duni wa wanachama | Kutotoa taarifa, kutojihusisha, au kutofuata taratibu za uanachama | Juu | Viashiria vya utendaji, motisha, mafunzo ya uelewa wa mtandao |
| 10 | Pengo la kidijitali | Kutotumia vizuri teknolojia kwenye ufuatiliaji na uratibu | Wastani | Mafunzo ya TEHAMA, vifaa vya gharama nafuu, mfumo wa taarifa za kisheria mtandaoni |

| Na. | Hatari | Maelezo | Kiwango cha Athari | Mikakati ya Kukabiliana |
|---|---|---|---|---|
| 11 | Kuondoka kwa wafanyakazi | Kupotea kwa kumbukumbu na uwezo wa kitaasisi | Chini | Mipango ya urithi (succession), mfumo wa usimamizi wa maarifa |



# 4. Rasilimali na Uendelevu

**4.0. Mkakati wa Uhamasishaji wa Rasilimali na Uendelevu**

Ili kutekeleza mpango huu wa kimkakati kwa ufanisi na kuongeza athari ya muda mrefu, TAPANET inahitaji kuwa na mikakati madhubuti ya uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali. TAPANET inatambua kuwa utegemezi mkubwa kwa wafadhili wachache ni tishio kwa uendelevu wake. Hivyo, mtandao huu utachukua mbinu ya kimkakati ya kuwa na vyanzo vingi vya fedha, sambamba na ndoto yake ya kuwa harakati ya msaada wa kisheria inayojiendesha, inayomilikiwa na wanachama, na yenye mizizi kwenye jamii.

Malengo ya Mkakati wa Uhamasishaji Rasilimali:

i. *Kuongeza vyanzo vya mapato vya TAPANET ili kupunguza utegemezi kwa wafadhili wachache.*
ii. *Kuimarisha mifumo ya ndani ya kuzalisha mapato kupitia huduma na ushirikiano.*
iii. *Kuongeza uwezo wa wanachama wa TAPANET katika kutafuta rasilimali ngazi ya ndani na kikanda.*
iv. *Kuiweka TAPANET kama taasisi inayoaminika ya uwekezaji kwa ubunifu wa msaada wa kisheria.*

**4.1 Mikakati ya Uhamasishaji wa Rasilimali**

**4.1.1. Ushirikiano na Wafadhili Pamoja na taasisi za kutoa ruzuku**

TAPANET itaendeleza na kuimarisha mahusiano na washirika wa maendeleo waliopo kama LSF, DANIDA, EU, Enabel, sambamba na kutambua wafadhili wapya wa pande mbili na wa kimataifa. Mkakati wa ushirikiano na wafadhili utaandaliwa ili kulinganisha malengo ya TAPANET na vipaumbele

vya haki duniani kama SDG 16, usawa wa kijinsia na haki za binadamu..

*Shughuli kuu kutekeleza hili:*

- **i.** Kuandaa waraka wa kutangaza fursa za uwekezaji (funding prospectus) na nyenzo za kuwasilisha miradi.
- **ii.** Kuandaa mikutano ya mashauriano na wafadhili na maonesho ya ubunifu wa msaada wa kisheria.
- **iii.** Kuhakikisha utoaji wa taarifa bora za kifedha na simulizi za athari za kazi za TAPANET.

### 4.1.2. Ushirikiano na Sekta Binafsi (CSR)

TAPANET itafungua milango ya ushirikiano na sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kampuni za sheria, mashirika ya simu, taasisi za kifedha, na makampuni yenye mpango wa uwajibikaji kwa jamii (CSR) yanayopenda kuwekeza katika haki na ujumuishi.

*Shughuli kuu kutekeleza hili:*

- Kuandaa vifurushi vya uwekezaji vya CSR.
- Kulenga sekta zenye mwelekeo wa haki, uwezeshaji wa vijana, na usawa wa kijinsia.
- Kuanzisha miradi ya pamoja (co-branded) kwa faida ya pande zote mbili (TAPANET na mfadhili).

### 4.1.3. Mapato Kutoka kwa Wanachama na Michango ya Ndani

Ukiwa ni mtandao wenye mashirika zaidi ya 170, TAPANET itaanzisha mfumo wa michango ya uanachama kulingana na uwezo wa kila shirika. Wanachama pia watahamasishwa kutoa huduma kwa njia ya kujitolea, kushirikiana katika uhamasishaji wa rasilimali, na kugharamia baadhi ya mafunzo na mikutano.

*Shughuli kuu kutekeleza hili:*

- Kurekebisha na kurasimisha sera ya michango ya uanachama.
- Kuweka gharama kwa baadhi ya huduma za kujenga uwezo zinazotolewa na TAPANET.
- Kuwazawadia wanachama wanaozingatia taratibu kupitia utangazaji na upatikanaji wa fursa maalum.

### 4.1.4. Huduma Zinazolipiwa na Uzalishaji wa Maarifa (ujengaji uwezo)

TAPANET itatumia utaalamu wake kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu (consultancy), mafunzo ya elimu ya kisheria, utayarishaji wa mtaala wa wasaidizi wa kisheria, na kutoa huduma za kubadilishana maarifa kwa taasisi za serikali, NGOs na wahisani.

*Shughuli kuu kutekeleza hili:*

- Kupanga na kuweka bei ya moduli na zana za mafunzo zitakazotolewa na TAPANET.
- Kuchapisha na kuuza vitini vya mafunzo kuhusu haki ya jamii, uelewa wa sheria, na mwitikio wa GBV.
- Kuanzisha kituo cha kujifunza kuhusu msaada wa kisheria kwa ada maalum kwa makundi maalum.

**4.1.5. Harambee (Uchangishaji) wa Rasilimali Ngazi ya Jamii**

TAPANET inatambua nguvu ya umiliki wa jamii kwa kuendeleza kampeni za uchangishaji kupitia matukio ya hisani, misafara ya haki (justice caravans), na michango kwa njia ya simu kwa ajili ya msaada wa kisheria katika maeneo yasiyohudumiwa.

*Shughuli kuu kutekeleza hili:*


- Kuandaa mwongozo wa kampeni ya uchangishaji wa rasilimali ngazi ya jamii kwa wanachama.
- Kuanzisha wiki za haki katika jamii zenye udhamini wa wadau wa ndani.
- Kutumia mifumo ya simu kama M-Pesa kwa kupokea michango kutoka kwa wananchi.

**4.1.6. Kuanzishwa kwa Mfuko bunifu wa Msaada wa Kisheria**

TAPANET itatetea kuanzishwa kwa mfumo wa pamoja wa fedha—Mfuko wa Ubunifu wa Msaada wa Kisheria—kwa ajili ya kusaidia miradi midogo ya wanachama katika maeneo kama huduma za kisheria za kidijitali, haki jumuishi ya kijinsia, na elimu ya sheria kwa vijana.

*Shughuli kuu kutekeleza hili*:

- Kubuni mfumo wa mfuko huo kwa kushirikiana na wafadhili na sekta binafsi.
- Kukuza upatikanaji wa mfuko huo kwa njia ya mashindano ya mapendekezo.
- Kufuatilia na kuonyesha mafanikio ya ubunifu huo kwa lengo la kuyaiga.



# 5. Mfumo wa Utekelezaji

### 5.0 Mpango wa Utekelezaji

Ili kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa vipaumbele vya Mkakati wa TAPANET, mpango wa utekelezaji unaoambatana na Hati ya Kiambatisho Na. 02 umeandaliwa ukieleza shughuli kuu, wadau wa utekelezaji, muda wa utekelezaji, na matokeo yanayotarajiwa.

Mpango Mkakati wa 2025–2029 umejikita katika nguzo tatu kuu:

i. **Kuimarisha uwezo wa watoa msaada wa kisheria (paralegals),**
ii. **Kuchechemuza mabadiliko ya sera na mifumo rafiki ya kisheria,**
iii. **Kujenga uendelevu wa shirika.**

*Nguzo ya Kwanza: Kuimarisha Uwezo wa Paralegals:* TAPANET itatekeleza mafunzo ya kisheria ya kitaalamu, kuzindua mfumo wa kitaifa wa uthibitisho wa paralegals, kukuza mfumo wa ulezi (mentorship), na kutumia TEHAMA kuboresha utoaji wa huduma. *Nguzo ya Pili: Uchechemuzi wa Mifumo Rafiki ya Kisheria*: Mtandao utaongoza mijadala ya sera, kusukuma kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Msaada wa Kisheria, kuendesha kampeni za uhamasishaji kuhusu haki, na kushiriki katika kuingiza paralegals katika mifumo rasmi ya utatuzi wa migogoro.

*Nguzo ya Tatu: Uendelevu wa TAPANET*: TAPANET itabuni mkakati wa kifedha, kuimarisha utawala wa

ndani, kuweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini (M&E), kupanua majukwaa ya kidijitali, na kuimarisha ushirikishwaji wa wanachama kupitia miongozo ya uandikishaji, programu za kutambua mchango wa wanachama, na mifumo ya mrejesho.

Kila hatua katika mkakati huu ina muda maalum wa utekelezaji, majukumu yaliyogawiwa kwa wadau husika, na matokeo yanayotarajiwa, ili kuhakikisha utekelezaji wenye mafanikio. Ramani hii ya kimkakati inalenga kuimarisha taaluma ya msaada wa kisheria, kuongeza upatikanaji wa haki, na kuimarisha uwezo wa TAPANET kuongoza harakati za paralegal nchini Tanzania kwa njia endelevu na yenye matokeo makubwa.

.


**Jedwari 2: Mpango wa Utekelezaji**

| Kipaumbele cha Kimkakati | Shughuli Kuu | Wadau Wanaohusika | Muda | Matokeo Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha uwezo na taaluma ya wasaidizi wa kisheria Kuandaa na kutekeleza mfumo wa uthibitisho wa kitaifa wa wasaidizi wa kisheria Kuanzisha programu za ushauri na ujifunzaji rika (peer learning) Kujumuisha zana za | Kuendesha mafunzo maalum ya msaada wa kisheria, haki za binadamu, na usawa wa kijinsia kwa wasaidizi | Sekretariati ya TAPANET, wataalamu wa sheria, taasisi za mafunzo | Endelevu | Kuongezeka kwa taaluma na ubora wa huduma za msaada wa kisheria |
| | TAPANET, MoCLA, taasisi za msaada wa kisheria | 2025–2026 | Huduma za kisheria zilizo sanifishwa na kitaaluma | |
| | TAPANET, wasaidizi wakongwe, NGOs | 2025–2029 | Kuimarika kwa usambazaji wa maarifa na ukuaji wa taaluma | |

| Kipaumbele cha Kimkakati | Shughuli Kuu | Wadau Wanaohusika | Muda | Matokeo Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|---|
| kidijitali kwa ajili ya usimamizi wa kesi na mafunzo | TAPANET, wabia wa TEHAMA, wafadhili | 2026–2029 | Kuongezeka kwa ufanisi na ufuatiliaji wa msaada wa kisheria | |
| Uchechemuzi kwa mazingira bora ya kisheria na kisera | Kufanya majadiliano ya sera na serikali ili kutambua rasmi wasaidizi wa kisheria | TAPANET, MoCLA, AZAKI | 2025–2027 | Kuongezeka kwa usaidizi wa serikali na utambuzi wa wasaidizi |
| Kutetea kuanzishwa kwa mfuko wa kitaifa wa msaada wa kisheria<br>Kuandaa kampeni za uchechemuzi za kitaifa na kikanda kuhusu upatikanaji wa haki | TAPANET, wafadhili, taasisi za serikali | 2025–2029 | Rasilimali za kifedha kwa ajili ya huduma za msaada wa kisheria | |
| Kuwezesha ushirikiano kati ya wasaidizi wa kisheria na mifumo ya | TAPANET, vyombo vya habari, AZAKI | Kila mwaka | Kuongezeka kwa uelewa wa umma na ushawishi wa kisera | |
| | TAPANET, mahakama, vyama vya sheria | 2026–2029 | Kuimarika kwa ushirikiano katika mfumo wa | |

| Kipaumbele cha Kimkakati | Shughuli Kuu | Wadau Wanaohusika | Muda | Matokeo Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|---|
| mahakama (ADR) | | | haki | |
| Uendelevu wa TAPANET na ufanisi wa huduma | Kuandaa mpango wa uendelevu wa kifedha wenye vyanzo mbalimbali vya rasilimali | TAPANET, wafadhili, sekta binafsi | 2025–2027 | Kupungua kwa utegemezi wa wafadhili na kuongezeka kwa ufadhili |
| Kutekeleza mfumo madhubuti wa M&E kwa ajili ya kupima athari | TAPANET, wataalamu wa M&E | 2026–2029 | Maamuzi yanayotegemea takwimu na uwajibikaji | |
| Kuimarisha muundo wa utawala na uongozi wa ndani | TAPANET, bodi, timu za ujenzi wa uwezo | 2025–2027 | Kuongezeka kwa ufanisi wa shirika na uongozi bora | |
| Kupanua majukwaa ya kidijitali kwa ajili ya huduma za msaada wa kisheria kwa njia ya mbali | TAPANET, wabunifu wa TEHAMA, NGOs | 2026–2029 | Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria | |
| Kufanya kampeni za usajili wa wanachama wapya Kuweka programu | TAPANET, mitandao ya wasaidizi wa kisheria | 2025–2029 | Kuongezeka kwa wanachama wa | |

| Kipaumbele cha Kimkakati | Shughuli Kuu | Wadau Wanaohusika | Muda | Matokeo Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|---|
| rasmi za mapokezi na maelekezo kwa wanachama wapya Kuweka utaratibu wa kutambua wanachama waliotoa mchango bora Kutekeleza mifumo ya maoni ya wanachama kuhusu huduma za mtandao | | | TAPANET | |
| | TAPANET, timu za mafunzo | 2026–2029 | Ushiriki mkubwa wa wanachama na kupungua kwa utoro wa wanachama | |
| | TAPANET, wafadhili, vyombo vya habari | 2026–2029 | Kuongezeka kwa motisha na uaminifu wa wanachama | |
| | TAPANET, mashirika wanachama | Endelevu | Uboreshaji unaotokana na mrejesho wa wanachama | |



# 6. Matokeo (Athari)

## 6.0. JINSI YA KUPIMA MATOKEO YETU (ATHARI)

Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) utakuwa sehemu muhimu ya mafanikio ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa TAPANET wa 2025–2029. Mfumo huu utawezesha Mtandao kufuatilia maendeleo, kuhakikisha uwajibikaji, kutathmini ufanisi wa shughuli, na kuongoza maamuzi kwa kuzingatia ushahidi.

Mfumo mpana wa M&E utaandaliwa ili kutekeleza mkakati huu kwa vitendo, ukiwa na viashiria wazi, viwango vya msingi (baselines), malengo ya kila mwaka, na zana za ukusanyaji wa data zinazoendana na malengo ya kimkakati na mfumo wa matokeo wa TAPANET.

Utekelezaji wa Mpango Mkakati utafuatiliwa kwa kipindi maalum kupitia ripoti za maendeleo, maoni ya wanachama, na mashauriano na wadau. Mapitio ya kila mwaka na ya kati ya kipindi (mid-term) yatafanyika ili kupima utendaji, kunasa mafunzo, na kuboresha mbinu za utekelezaji. Katika ngazi ya taasisi, utendaji utapimwa kwa kutumia viashiria muhimu vya matokeo vilivyoainishwa ndani ya Mpango Mkakati, huku mafunzo ya kitaasisi na mrejesho kutoka kwa wanachama yakiongoza maamuzi ya mipango mikubwa.

Zaidi ya hayo, mapitio ya kati na ya mwisho ya utekelezaji wa Mpango Mkakati yatafanyika ili kupima kiwango kamili cha utekelezaji na athari yake kwa ujumla. Mapitio haya yatazalisha ushahidi wa kuongoza utekelezaji wa mpango katika miaka inayofuata na kuchangia kwenye maandalizi ya Mpango Mkakati wa TAPANET unaofuata.

Ili kuimarisha hili, TAPANET itaboresha Mfumo wake wa Usimamizi wa Utendaji ili kufuatilia mchango wa kila mfanyakazi mmoja mmoja na kuhakikisha unaendana na vipaumbele vya kimkakati. Mbinu hii ya ngazi mbili — taasisi na mtu binafsi — itahakikisha mshikamano kati ya shughuli za kila siku na matokeo ya muda mrefu.

Hatimaye, mfumo wa M&E utatumika kama chombo cha kujifunza na dira ya kimkakati, kikiiwezesha TAPANET kutoa matokeo yanayopimika ya haki kwa jamii mbalimbali nchini Tanzania.

### 6.1. Viashiria Muhimu vya Utendaji (Key Performance Indicators - KPIs)

Mpango Mkakati unajumuisha mfumo madhubuti wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) ukiwa na Viashiria Muhimu vya Utendaji (KPIs) vilivyobuniwa kufuatilia maendeleo katika maeneo yote ya kimkakati. Kwa ajili ya kuimarisha taaluma ya paralegals, KPIs zitahusisha idadi ya paralegals waliofundishwa na kuthibitishwa, programu za ulezi (mentorship) zilizotekelezwa, na vikao vya uelimishaji wa kisheria kwa jamii—ambavyo vitapimwa kupitia kumbukumbu za mafunzo na mrejesho.

Ufanisi wa uchechemuzi utapimwa kwa idadi ya mageuzi ya sera yaliyoshawishiwa, kampeni zilizoendeshwa, ushiriki wa vyombo vya habari, na ongezeko la ufadhili wa msaada wa kisheria kutoka serikalini. Uendelevu wa shirika utapimwa kwa kupitia utofauti wa vyanzo vya wafadhili, ongezeko la fedha, ufanisi wa kiutendaji kupitia matumizi ya TEHAMA, na kiwango cha ushiriki wa wanachama. TAPANET pia itafuatilia utekelezaji wa viwango vya ubora wa huduma, ongezeko la wanachama, ushiriki wa wanachama, na viwango vya kubaki kwenye mtandao (retention).

Juhudi za uhamasishaji wa rasilimali zitafuatiliwa kupitia dashibodi za kifedha, taarifa za michango kutoka kwa wafadhili, na ufuatiliaji wa ulinganifu wa michango ya wanachama. Viashiria hivi kwa pamoja vitahakikisha maamuzi yanayotegemea ushahidi na kuiwezesha TAPANET kupima utendaji, kuonesha matokeo, na kurekebisha mikakati ili kuboresha upatikanaji wa haki kote nchini.

**Jedwari 3: Mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini**

| Eneo la Kimkakati | Viashiria Vikuu vya Utendaji (KPIs) | Vipimo vya Upimaji (Measurement Metrics) |
|---|---|---|
| Kuimarisha uwezo na taaluma ya wasaidizi wa kisheria | - Idadi ya wasaidizi wa kisheria waliopatiwa mafunzo kila mwaka | Rekodi za vikao vya mafunzo, vyeti vilivyotolewa |
| | - Asilimia ya wasaidizi wa kisheria waliothibitishwa kupitia mfumo wa kitaifa | Kazidata ya uthibitisho, uzingatiaji wa kanuni |
| | - Idadi ya programu za ushauri na ujifunzaji wa rika | Ripoti za ushiriki wa mentorship |
| | - Kuongezeka kwa kampeni za uelewa wa sheria kwa jamii | Idadi ya vipindi vya elimu ya sheria, mrejesho kutoka kwa jamii |

| Eneo la Kimkakati | Viashiria Vikuu vya Utendaji (KPIs) | Vipimo vya Upimaji (Measurement Metrics) |
| --- | --- | --- |
| **Uhamasishaji wa Rasilimali** *(utafuatiliwa kupitia dashibodi za kifedha za kila robo mwaka, rejista za wafadhili, na taarifa za michango ya wanachama)* | - - Idadi ya wafadhili hai | Ripoti za wafadhili |
| | - Jumla ya mapato kulingana na aina ya chanzo cha fedha | Ripoti za wafadhili |
| | - Asilimia ya ongezeko la fedha zisizo na masharti maalum | Ripoti za wafadhili |
| | - Kiwango cha ufuataji wa michango ya wanachama | kanzidata ya wanachama |
| uchechemuzi kwa mazingira wezeshi ya kisheria na kisera | - dadi ya mageuzi ya sheria na sera yaliyochangiwa na TAPANET | Ripoti za serikali, kumbukumbu za mabadiliko ya sera |
| | - Idadi ya kampeni za uchechemuzi zilizofanyika | Ripoti za matukio ya uchechemuzi, rekodi za ushirikiano wa wadau |
| | - Ongezeko la msaada wa kifedha kutoka serikalini kwa huduma za msaada wa kisheria | Mgawanyo wa bajeti, ripoti za ufadhili wa msaada wa kisheria |
| | - Idadi ya ushirikiano na vyombo vya habari na kampeni za uhamasishaji | Taarifa kwa vyombo vya habari, uchambuzi wa uandishi wa habari |
| Kuhakikisha uendelevu wa TAPANET na utoaji wa huduma bora | - Kuongezeka kwa vyanzo vya fedha na utofauti wa wafadhili kila mwaka | Taarifa za kifedha, mikataba ya ushirikiano |
| | - Asilimia ya ongezeko la ufanisi kupitia matumizi ya TEHAMA katika huduma za msaada wa kisheria | Rekodi za mahudhurio ya mikutano, ripoti za mrejesho |
| | - Idadi ya shughuli za ushiriki wa wanachama zinazofanyika kila mwaka | Meeting attendance records, feedback reports |

| Eneo la Kimkakati | Viashiria Vikuu vya Utendaji (KPIs) | Vipimo vya Upimaji (Measurement Metrics) |
|---|---|---|
| | - Utekelezaji wa viwango vya ubora wa huduma kwa wanachama wote wa TAPANET | Ripoti za ukaguzi wa uzingatiaji, tathmini za ubora wa huduma |
| | - Ukuaji wa wanachama wa TAPANET ndani ya kipindi cha miaka mitano | Rejista ya wanachama, rekodi za ushiriki |
| | - Asilimia ya wanachama wanaoshiriki kikamilifu kwenye programu za TAPANET | Rekodi za ushiriki wa matukio, tafiti za mrejesho |
| | - Kupungua kwa viwango vya kuondoka kwa wanachama | Taarifa za uhifadhi wa wanachama, ripoti za mahojiano ya kutoka (exit interviews) |
| | - Idadi ya programu za maendeleo ya taaluma na utambuzi wa wanachama | Rekodi za mafunzo, rekodi za tuzo na motisha |

Ili kuimarisha uwajibikaji, TAPANET itaweka viashiria vya msingi (baseline) kwa mwaka 2025 kwa baadhi ya viashiria muhimu vya utendaji (KPIs), na kuweka malengo ya hatua kwa hatua kwa mwaka 2027 na 2029. Hii itaiwezesha TAPANET kufuatilia mwenendo wa utekelezaji, kurekebisha programu zake kwa wakati, na kutoa taarifa kwa uwazi kwa wanachama na wadau wengine.

### 6.2. Mapitio ya Kila Mwaka na Utoaji wa Taarifa

- Mapitio ya utendaji ya kila mwaka: TAPANET itafanya tathmini za kila mwaka kwa muundo maalum ili kupima ufanisi wa mikakati yake, kufuatilia maendeleo dhidi ya viashiria vya utendaji (KPIs), na kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa.
- Ripoti za ufuatiliaji za kila robo mwaka: Ufuatiliaji wa utekelezaji kwa wakati utahakikisha TAPANET inaweza kujibu changamoto na fursa kwa haraka.
- Tafiti kwa wanachama na wadau: TAPANET itakusanya mrejesho kutoka kwa mashirika ya wasaidizi wa kisheria, taasisi za serikali, na wafadhili ili kusaidia katika maamuzi ya kimkakati.

- Tathmini huru ya athari: Uhakiki wa nje utafanyika ili kupima athari ya jumla ya kazi na mipango ya TAPANET.

## 6.3. Vipimo vya Ushiriki wa Wadau

- Idadi ya ushirikiano ulioanzishwa na taasisi za serikali, AZAKI na wafadhili
- Viwango vya kuridhika kwa wadau kama vinavyopimwa kupitia tafiti za ushiriki
- Marudio na ubora wa mikutano ya mashauriano na watunga sera na taasisi za sheria
- Kuongezeka kwa mwonekano na ufanisi wa TAPANET katika uchechemuzi (kupimwa kwa kupitia kutajwa na vyombo vya habari na ushawishi wa sera)

## 6.4. Vipimo vya Uhamasishaji wa Rasilimali

- Idadi ya wafadhili hai
- Jumla ya mapato kulingana na aina ya chanzo cha fedha
- Asilimia ya ongezeko la fedha zisizo na masharti maalum (unrestricted/core funding)
- Kiwango cha ufuataji wa michango ya wanachama

Kwa kuunganisha Viashiria vya Utendaji (KPIs), vipimo vya mafanikio, na mifumo ya tathmini ya athari, TAPANET itahakikisha uwajibikaji, kujifunza kwa mfululizo, na uwezo wa kujiimarisha katika utekelezaji wa dhamira yake. Mbinu hii ya kimfumo itasaidia katika kufanya maamuzi yanayoongozwa na takwimu, hivyo kuimarisha nafasi ya TAPANET katika kuboresha huduma za msaada wa kisheria na upatikanaji wa haki nchini Tanzani.